



Storybooks Canada

storybookscanada.ca


Nozibele na nywele tatu / Nozibele and
the three hairs

Written by: Tessa Welch

Illustrated by: Wiehan de Jager

Translated by: (sw) Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook
(africanstorybook.org) and is brought to you by
Storybooks Canada in an effort to provide
children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



Nozibele na nywele tatu

Nozibele and the three hairs



✎ Tessa Welch

🔊 Wiehan de Jager

📖 Matteo E. Mwita

💬 Kiswahili / English

📖 Level 3



Hapo zamani za kale, wasichana watatu walienda kukusanya kuni.

...

A long time ago, three girls went out to collect wood.



Mbwa akagundua kuwa Nozibele amemkimbia. Kwa hiyo akakimbia kuelekea kijijini. Kaka zake Nozibele walikuwa wakimsubiri na fimbo. Mbwa alipowaona akageuka na kukimbia, na hajawahi kuonekana tena.

...

Then the dog knew that Nozibele had tricked him. So he ran and ran all the way to the village. But Nozibele's brothers were waiting there with big sticks. The dog turned and ran away and has never been seen since.



Ilikuwa ni siku yenye jua kali na wakaamua kwenda mtoni kuogelea. Wakaogelea huku wakicheza na kurushiana maji.

...

It was a hot day so they went down to the river to swim. They played and splashed and swam in the water.



Ghafla waligundua kuwa muda umekwenda.
Wakaharakisha kurudi nyumbani.

...

Suddenly, they realised that it was late. They hurried
back to the village.



Mbwa aliporudi akaanza kumtafuta Nozibele. "Nozibele,
uko wapi?" akapiga kelele. "Niko hapa, chini ya kitanda,"
unywele wa kwanza ukajibu. "Nipo hapa nyuma ya
mlango," unywele wa pili ukajibu. "Niko hapa kwenye
uzio," unywele wa tatu ukajibu.

...

When the dog came back, he looked for Nozibele.
"Nozibele, where are you?" he shouted. "I'm here, under
the bed," said the first hair. "I'm here, behind the door,"
said the second hair. "I'm here, in the kraal," said the
third hair.



Mara baada tu ya mbwa kuondoka, Nozibele akanyofoa nywele tatu kutoka kwenye kichwa chake. Akaweka unywele mmoja chini ya kitanda, mmoja nyuma ya mlango, na mwingine akaweka kwenye uzio wa nyumba. Halafu, akakimbia kuelekea nyumbani kwa nguvu zote.

...

As soon as the dog had gone, Nozibele took three hairs from her head. She put one hair under the bed, one behind the door, and one in the kraal. Then she ran home as fast as she could.



Walipokuwa wanakaribia kufika nyumbani, Nozibele akajishika shingoni. Alikuwa amesahau shanga zake! "Tafadhali turudini!" aliwasihi rafiki zake. Lakini rafiki zake wakasema tumechelewa.

...

When they were nearly home, Nozibele put her hand to her neck. She had forgotten her necklace! "Please come back with me!" she begged her friends. But her friends said it was too late.



Kwa hiyo Nozibele akarudi mwenyewe mtoni. Akapata shanga zake na akakimbia kurudi nyumbani. Lakini akapotea gizani.

...


So Nozibele went back to the river alone. She found her necklace and hurried home. But she got lost in the dark.



Akawa kila siku anampikia, anamfulia na kumfagilia mbwa. Siku moja mbwa akasema, "Nozibele, leo naenda kuwatembelea rafiki zangu. Fagia nyumba, pika chakula na osha vitu vyangu kabla sijarudi."

...

Every day she had to cook and sweep and wash for the dog. Then one day the dog said, "Nozibele, today I have to visit some friends. Sweep the house, cook the food and wash my things before I come back."



Mbwa akawwambia, "Nitandikie kitanda!" Nozibele akajibu, "Sijawahi kumtandikia mbwa kitanda." "Tandika kitanda, la sivyo nitakung'ata!" mbwa akasema. Nozibele akatandika kitanda.

...

Then the dog said, "Make the bed for me!" Nozibele answered, "I've never made a bed for a dog." "Make the bed, or I'll bite you!" the dog said. So Nozibele made the bed.



Kwa mbali akaona mwanga unatoka kwenye nyumba. Akakimbilia kwenye nyumba na kugonga mlango.

...


In the distance she saw light coming from a hut. She hurried towards it and knocked at the door.



Akastaajabu kumwona mbwa akifungua mlango na akasema, “Unataka nini?” “Nimepotea na ninatafuta sehemu ya kulala,” akasema Nozibele. “Ingia ndani, la sivyo nitakung’ata!” mbwa akamwambia. Nozibele akaingia ndani.

...

To her surprise, a dog opened the door and said, “What do you want?” “I’m lost and I need a place to sleep,” said Nozibele. “Come in, or I’ll bite you!” said the dog. So Nozibele went in.



Mbwa akamwambia, “Nipikie!” “Sijawahi kumpikia mbwa,” akajibu. “Pika, la sivyo nitakung’ata!” mbwa akasema. Nozibele akampikia mbwa chakula.

...

Then the dog said, “Cook for me!” “But I’ve never cooked for a dog before,” she answered. “Cook, or I’ll bite you!” said the dog. So Nozibele cooked some food for the dog.